



# Now | Next

Worcester's Citywide Plan

Muhtasari Mkuu

# Muhtasari Mkuu

Worcester ya Sasa | ya Baadaye ni mpango wa muda mrefu wa Jiji zima la Worcester. Unaonyesha maono na maadili ya jumuiya yetu na kutoa mfumo wa kuongoza jinsi tunavyowekeza na kutengeneza jiji letu katika miaka 10 ijayo, hasa katika suala la maendeleo na miundombinu. Kwa kutumia mfumo huu, mipango ya baadaye ya mada na ya sehemu mahususi itafungamana pamoja ili kufikia zaidi ya vile mpango wowote mmoja ungefikia ukiwa peke yake.

Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu mpango huu katika [now-next.worcesterma.gov](http://now-next.worcesterma.gov)

## Mchakato

Katika kipindi cha miaka miwili, kuanzia mapema 2022 hadi mapema 2024, mchakato wa Worcester ya Sasa | ya Baadaye uliwashirikisha wanajumuiya na wadau mbalimbali katika uundaji wa pamoja wa mpango ambao unaweza kuakisi matarajio na mahitaji ya jumuiya ya Worcester sasa, na katika sura inayofuata ya jiji. Mchakato huu ulijikita katika kazi ya mratibu wa jumuiya ya eneo la watu wanaozungumza lugha mbili, anayefanya kazi kwa muda na ulijumuisha awamu mbili: awamu ya kuweka malengo na maono ambapo tulisikiliza na kupata maelezo ili kutambua masuala na fursa, na awamu ya utoaji wa mapendekezo na kuweka vipaumbele ambapo tulichambua maelezo ya jinsi ya kufikia maono na malengo yaliyojitokeza kutoka kwa awamu ya kuweka malengo na maono.

### Maono

**Katika karne ya nne ya Worcester, tunatazamia jiji bunifu la watu wanaothamini ujumuishaji na kusherehekea uanuwai. Tutainua jiji letu kwa kuwekeza kwa usawa katika jumuiya zetu, kuunganisha vitongoji vyetu na fursa, na kuwekea kipaumbele ukuaji endelevu unaounga mkono maisha bora kwa wote.**



Kupitia kazi ya msingi ya mratibu wa eneo na ushirikiano na mashirika ya jumuiya, mchakato huu wa kupanga uliweza kujenga mtandao thabiti wa kusambaza maelezo na kubuni fursa za kushirikisha watu mahali walipo. Vipengele vyote vya juhudi za kushirikisha umma vilikuwa vya lugha mbili (Kiingereza na Kihispania), maelezo muhimu yalishirikiwa katika lugha 6 kuu katika Worcester (Kireno, Kitwi, Kivietinamu, Kiarabu, Kialbania, na Kiswahili), na warsha za umma zilirekebisha ili kuwafaa washiriki walio na ulemavu wa kusikia na wa kuona. Msingi huu thabiti ulituwezesha kupata maoni kutoka kwa wanajumuiya wa Worcester ambao mara nyingi huwa na uwakilishi mdogo katika michakato ya upangaji kama hii.

## Takwimu za ushirikishaji



Zaidi ya washiriki **780** waliosajiliwa kupokea jarida linalotumwa kwa barua pepe

### Awamu ya 1: Kuweka malengo na maono

Utafiti wa Mtandaoni wa Jiji Nzima wa Kuweka Malengo na Maono



Washiriki **1,377**



Taarifa **1,241** Ziliwasilishwa

Warsha za Umma za Kubuni Malengo na Maono



Zaidi ya Washiriki **100** Waliohudhuria



Maoni **755** Yaliyoandikwa

Ziara ya Kupokea Maoni ya Kuweka Malengo na Maoni



Viibukizi **13** vya Hafla ya Jumuiya



Zaidi ya Kadi **258** za Maono

Vikundi **3** vya Kupokea Maoni



### Awamu ya 2: Mapendekezo na Uwekaji wa Vipaumbele

Hojaji ya Malengo ya Kipaumbele



Majibu **1,030**

Warsha za Umma za Kutengeneza Rasimu na Maonyesho ya Maktaba



Zaidi ya Washirik **113** Waliohudhuria



Zaidi ya Washiriki **50** Waliohudhuria Ana kwa Ana



Washiriki **63** Walioshiriki Mtandaoni



Zaidi ya Maoni **150** Yaliyoandikwa



Kura **2,025** za Karatasi Zinazonata za Mapendekezo

## Vichwa vya Mpango

Vichwa vitatu vya mpango viliibuka kutokana na ushirikishwaji wa kina na uchambuzi uliofanywa kupitia mchakato huu wa upangaji. Vichwa hivi vinawakilisha kiini cha mpango, na kile ambacho mpango unaelekeza Jiji lichukulie hatua katika miaka michache ijayo.

**Mfumo unaozingatia maadili kwa ukuaji unaonufaisha wanajumuiya wote wa Worcester.**

**Uwekezaji sawa na endelevu wa umma katika vitongoji vya Worcester.**

**Jiji lililounganishwa zaidi na linalofikika na wote.**

### **Mfumo unaozingatia maadili kwa ukuaji unaonufaisha wanajumuiya wote wa Worcester.**

Worcester inakua na kubadilika kwa kasi. Mpango wa Worcester ya Sasa | ya Baadaye unatoa mkakati wa jinsi ya kushughulikia ukuaji na kudhibiti mabadiliko kwa njia inayoakisi maadili na malengo ya pamoja ya jumuiya. Tulisikia kuwa watu wanataka maendeleo yenye usawa, endelevu, na yenye kustahimili mabadiliko; chaguo anuwai zaidi za nyumba za bei nafuu ambazo zinashughulikia ipasavyo tatizo ya makazi; na vituo vizuri vya ujirani vya matumizi mseto na njia ambazo zinaweza kutembelewa na kufikiwa na watu wa kila umri na uwezo. Ili kufikia hilo na kuhakikisha kuwa ukuaji unaoendelea wa Worcester unanufaisha Watu wote wa Worcester katika vizazi vijavyo, tunahitaji upangaji upya wa maeneo, mpango wa hatua wa kushughulikia mapungufu ya kutoka sehemu moja hadi nyingine, na tathmini ya maboresho ya miundombinu yanayohitajika ili kusaidia ukuaji huo.

#### **Jinsi tunavyoendeleza hili:**

1. Kutekeleza masasisho maalum, yaliyolengwa ya maeneo ya masuala maalum kama vile (lakini sio tu) kuwezesha Vitengo vya Makazi

- ya Nyongeza (ADU), kupunguza masharti ya maegesho inapofaa, na kuweka masharti ya ulinzi na upanzi wa miti.
2. Kuanzisha marekebisho ya maeneo ili kuoanisha ramani ya maeneo na Mfumo wa Ukuaji ulioanzishwa kupitia mpango huu, ili kushughulikia vipengele vya sheria ya sasa ambavyo vinaendeleza ubaguzi na ukosefu wa usawa au kuathiri uwezekano wa maendeleo yanayotarajiwa katika jiji lote, na kuboresha uwazi na uzuri wa utumiaji wa sheria.
3. Kukamilisha na kutekeleza Mpango wa Hatua wa Uhamaji (MAP) ili kutambua na kuwekea kipaumbele miradi mahususi zaidi ya mtaji, uendeshaji, na mipango ili kuendeleza usafiri salama, sawa na endelevu katika Worcester ili kuunga mkono Mfumo wa Ukuaji.
4. Kukamilisha ujenzi wa miundombinu na tathmini za mahitaji ili kuthibitisha uwezo wa sasa wa miundombinu ya umeme, maji ya mvua, na mifereji ya maji taka na kutambua uwekezaji unaohitajika ili kusaidia Mfumo wa Ukuaji na Maono ya Matumizi ya Ardhi ya Baadaye yaliyoandaliwa kupitia mpango huu..

## **Uwekezaji sawa na endelevu wa umma katika vitongoji vya Worcester.**

Kulikuwa na utambuzi mkubwa kuwa Maeneo ya Chini na Wilaya ya Canal yanapaswa kuendelea kuwa maeneo muhimu ya kuzingatia kwa mipango, uwekezaji, upangaji, na mipango ya maendeleo ya ubunifu ambayo yanasaidia ubora wa katikati mwa jiji. Hata hivyo, mchango wa jumuiya katika mchakato huu wote wa upangaji ulionyesha shauku kubwa katika mwelekeo mpya wa vitongoji tofauti vya Worcester kupitia upangaji wa uratibu wa matumizi ya ardhi na miundombinu na uwekezaji wa kimkakati katika vitongoji, njia na wilaya zaidi ya katikati mwa jiji. Kwa usaidizi wa washirika wa jumuiya, Jiji limejitolea kutekeleza mipango ya ndani iliyoratibiwa, inayozingatia usawa, sera na uwekezaji wa umma ambayo kwa pamoja itaimarisha ubora wa vituo vya matumizi mseto ambavyo vinasaidia ubora wa maisha ya wakaazi na ustawi wa biashara ndogo ndogo.

### **Jinsi tunavyoendeleza hili:**

1. Upangaji wa ujirani na maeneo unaojumuisha matumizi ya ardhi, usafiri na mikakati ya

uwekezaji wa miundombinu ili kusaidia kikamilifu fursa za ujirani na ubora wa maisha.

2. Kupanga upya maeneo ili kuoanisha masharti ya udhibiti na maono na mapendekezo yanayotokana na upangaji wa ujirani na njia.
3. Kuweka kipaumbele kwa uwekezaji katika miundombinu na maendeleo ya kiuchumi katika vituo vya ujirani na njia kwa kuzingatia Mfumo wa Ukuaji.
4. Kuendelea na kupanua usaidizi dhidi ya uhamishaji kwa matumizi ya makazi na yasiyo ya makazi.
5. Kuboresha na kupanua rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa kanuni ili kushughulikia kwa vitendo masuala ya ufikiaji, afya na usalama katika nyumba za kukodisha na
6. Kutekeleza mabadiliko ya mchakato ili kuongeza ushiriki wa jumuiya na uwajibikaji katika mchakato ya maendeleo kupitia mabadiliko ya kiteknolojia na kiutaratibu ambayo yanaboresha uwazi na ujumuishwaji.

## **Jiji lililounganishwa zaidi na linalofikika na wote.**

Worcester ina utele wa mali, vituo vya huduma, na sehemu muhimu za jumuiya. Hata hivyo, ufikiaji wa vituo hivyo haulingani na unategemea sana magari. Miundombinu iliyopo ya uchukuzi inayotawaliwa na magari ya Worcester na mapengo yanayohusiana na uwekezaji katika miundombinu, vifaa na huduma zingine huzidisha ukosefu wa usawa katika ufikiaji na kuzidisha masuala ya afya ya umma na haki ya mazingira. Mpango huu unaashiria mabadiliko ya kuanza kuunda jiji lililounganishwa zaidi ambapo fursa za kiuchumi, huduma, na vituo vya huduma vinapatikana kwa wote kupitia uratibu wa matumizi ya ardhi na mipango ya uhamaji. Hasa, kupitia mchakato unaofuata wa upangaji wa MAP, Jiji litabainisha mbinu iliyoratibiwa, ya njia mbalimbali ya usafiri ambayo inaweka kipaumbele usalama, usawa na uendelevu huku ikikuza maendeleo ya jumuiya na kusaidia msongamano na mseto wa matumizi ya ardhi ulio katika Mfumo wa Ukuaji (angalia ukurasa unaofuata).

### **Jinsi tunavyoendeleza hili:**

1. Kusawazisha na kutekeleza mbinu bora za usimamizi katika vipimo na kanuni za Jiji zinazoathiri muundo, uendeshaji na shughuli

za mitaa ya umma, njia za kutembelea kando ya barabara na maeneo ya umma.

2. Kutekeleza mpango ulioratibiwa wa miradi ili kuboresha urahisi wa kutembea na ufikiaji, kuweka vipaumbele sehemu kama vile shule, njia zenye matumizi mengi, na maeneo ya mikusanyiko ya jumuiya.
3. Kufanya kazi na WRTA ili kupanua na kuboresha ubora, mzunguko, na ufikiaji wa huduma ya usafiri wa umma, hasa kwenye njia za kipaumbele na katika maeneo ambayo hayana huduma.
4. Kufanya kazi na MBTA ili kutoa huduma ya reli ya abiria ya mara kwa mara na inayoweza kutegemewa katika pande zote mbili, ikijumuisha treni nyingi za haraka za chini ya saa moja kati ya Boston na Worcester wakati wa idadi kubwa ya wasafiri.
5. Kutengeneza mtandao wa kina wa baiskeli na magari madogo unaounganisha maeneo yote ya jiji.
6. Kurejesha upya na kupanga upya mitaa ili kuwa salama na kuwa na sifa zinazofaa kwa mazingira yao ya mijini.
7. Kuunganisha matumizi ya ardhi na usafirishaji kupitia utengenezaji wa maeneo na uratibu wa juhudi za upangaji katika ngazi ya vitongoji.

## Mfumo wa Ukuaji

Worcester ilipata zaidi ya watu 25,000 katika miaka 10 iliyopita. Hii inawakilisha ongezeko la asilimia 14 na kupita kilele cha hapo awali cha idadi ya watu wa Worcester katika miaka ya 1950. Ingawa hatuwezi kujua ikiwa ukuaji utaendelea kwa kiwango sawa katika siku zijazo, tukiangazia mbele katika mwaka wa 2040, kiwango cha juu cha makadirio ya ukuaji wa idadi ya watu huko Worcester kinaweza kuwa wakazi wapya 60,000 au zaidi. Ili Worcester itoe makazi kwa watu hawa wengi, nyumba 20,000 au zaidi za familia nyingi zitahitajika.

Mfumo wa Ukuaji wa mahali maalum ulioundwa kupitia mchakato huu wa upangaji haushughuliki tu ukuaji ambao Worcester inaweza kupata katika miaka 20 ijayo, bali unaelekeza ukuaji huo pale ambapo ina uwezo mkubwa zaidi wa kufikia malengo ya jumuiya. Kwa kuelekeza ukuaji kwenye sehemu ambazo (au zilizo na uwezekano) wa kuwa na huduma nzuri za usafiri na vikundi vizuri vya vituo vya huduma, huduma na miundombinu ya ziada katika sehemu hizo, tunaweza kuunda Worcester inayofikika zaidi, yenye usawa, uendelevu, thabiti na inayokua zaidi.

Mfumo wa Ukuaji, kama unavyoonyeshwa kwenye ramani kwenye ukurasa ulio upande wa pili wa ukurasa huu, una kategoria au aina nne za ukuaji ambazo zitasaidia kwa pamoja kuanzisha muundo wa maendeleo unaozingatia njia za kupita na unaowezesha watu kutembea kwa urahisi ambao unaweza kuwezesha ubora wa juu wa maisha huku ukistahimili ukuaji mkubwa:

### Ukuaji wa Kimsingi wa Jiji Lote

Unawezesha ukuaji wa ziada, kidogo katika kila sehemu ya jiji.

### Maeneo ya Ukuaji Unaosimamiwa

Unawezesha ongezeko la wastani la idadi ya nyumba ndani ya umbali wa kutembea wa robo maili kutoka kwa njia zilizopo na zinazoweza kuwekwa baadaye.

### Maeneo ya Ukuaji wa Mabadiliko


Huwezesha maendeleo ya ziada ya matumizi mseto kwenye mali zilizo wazi au zisizotumika vizuri katika maeneo yaliyopo yenye uwezo wa juu wa kutembea na ufikiaji wa usafiri.

### Maeneo ya Ukuaji wa Mabadiliko

Huwezesha uwekezaji mkubwa na mabadiliko ya kimaumbile katika maeneo ambayo hayajafikiwa na uwezo mkubwa wa kutembea na ufikiaji wa usafiri ambayo yanaweza kusaidia ukuaji mkubwa wa kazi na/au makazi yenye watu wengi zaidi yenye matumizi ya ziada ya kibiashara.

Ili kufikia uwezo wao kamili kama vitovu vya matumizi mseto vinavyostawi vilivyotazamiwa kupitia mpango wa Worcester ya Sasa | ya Baadaye, Maeneo ya Ukuaji wa Mabadiliko yatapelewa kipaumbele kwa:

- Upangaji wa kiwango cha wilaya ili kufafanua malengo ya kina zaidi na masharti ya jumuiya katika kila eneo kuhusiana na kanuni za matumizi ya ardhi, uwekezaji wa mtaji, na mahitaji ya mpango au ya uendeshaji. Upangaji huu unapaswa kusaidia kueleza maono thabiti ya muundo wa miji ambayo yanawiana na uwekezaji unaotarajiwa wa miundombinu na vigezo vya matumizi ya ardhi.
- Uwekezaji maalum katika usalama na starehe ya watu wanaotembea kwa miguu, ufikiaji, miundombinu ya usafiri wa aina mbalimbali, na huduma bora ya usafiri wa umma kama ilivyobainishwa kupitia MAP.
- Uwekezaji wa mtaji ulioratibiwa katika miundombinu, huduma, na nyenzo, ikijumuisha uwekezaji muhimu unaohitajika wa watoa huduma wa mashirika ya kibinafsi (k.m. Gridi ya Kitaifa/Eversource).




Mfumo wa Ukuaji utakuwa msingi wa upangaji upya wa maeneo ya jiji lote katika siku zijazo pamoja na juhudi za upangaji wa maeneo, kuanzia katika Maeneo ya Ukuaji wa Mabadiliko.

- Maeneo ya Chini na Wilaya ya Canal
- Maeneo ya Ukuaji Unaoleta Mageuzi
- Maeneo ya Ukuaji ya Kujazia
- Maeneo ya Ukuaji Unaosimamiwa—Njia Iliyopo ya Usafiri
- Maeneo ya Ukuaji Unaosimamiwa—Njia za Usafiri Zinazowezekana Kuwepo katika Siku Zijazo

## Maono ya Baadaye ya Matumizi ya Ardhi

Maendeleo yote hayafanani. Baadhi ya matumizi yanaoana na kukamilishana (kama vile matumizi ya makazi na maduka ya rejareja) na mengine yanahitaji umbali zaidi na kuakibishwa kutoka kwa nyingine (kama vile makazi na matumizi ya viwanda yenye athari kubwa). Kwa kueleza ni matumizi gani ya mseto ambayo kila Eneo la Ukuaji wa Ujazo na Mabadiliko linafaa zaidi, Worcester inaweza kusaidia kuendeleza maendeleo ili kuunda mseto wa manufaa kwa pande zote mbili na kuimarisha ulinzi na utengano inapohitajika.

Kategoria zote za matumizi ya baadaye ya ardhi huruhusu matumizi mseto, lakini kwa matumizi tofauti kuu na matumizi ya ziada. Kategoria hizi kwa ujumla huelezea mseto wa matumizi ulio na msingi wa matumizi yaliyoangaziwa katika jina la kategoria na kuungwa mkono na mseto wa matumizi. Mara nyingi, kuna mchanganyiko wenye nguvu uliopo wa matumizi ambao hutofautiana na maono ya matumizi ya ardhi yaliyotambuliwa; maono haya yanajumuisha matumizi hayo yaliyopo na kuangazia jinsi mseto huo wa matumizi unavyoweza kubadilika baada ya muda ili kunufaika vyema na mifumo ya kipekee, viambajengo, na uwezo wa ukuaji wa kila eneo.





- **Matumizi Mseto:** Kwa kawaida huwa na msingi wa ghorofa ya chini ya biashara inayotumika (k.m. rejareja, burudani, na huduma kama vile benki, vinyozi, au kusafisha kavu), zenye ghorofa za juu za makazi na ofisi.
- **Sayansi ya Maisha:** Kwa kawaida huwa na msingi wa watoa huduma za afya, utafiti wa kisayansi, na matumizi ya maabara ya maendeleo, pamoja na rejareja, biashara, hoteli, taasisi za elimu na makazi machache ya ziada.
- **Ufundi:** Kwa kawaida huwa na msingi wa watengenezaji wadogo na wabunifu wenye athari ya chini (k.m. mitindo, samani, vyakula na vinywaji), pamoja na rejareja, biashara, hoteli na makazi.
- **Viwandani:** Kwa kawaida huwa na msingi wa wazalishaji na wasambazaji wakubwa wanaotumia malori makubwa, barabara kuu, na reli, pamoja na sehemu ndogo ya biashara na rejareja ya biashara na wafanyakazi wa eneo hilo.

## Vipaumbele vya Utekelezaji

Kwa miaka 3-5 ijayo, vipengee sita vifuatavyo vilivyopewa kipaumbele cha hatua za mapema vitakuwa lengo kuu la Kitengo cha Huduma za Mipango na Udhibiti ndani ya Ofisi ya Mtendaji Mkuu ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Jiji la Worcester. Vitendo hivi vya kipaumbele vya mapema vinavyoongozwa na Jiji vimeorodheshwa takriban kwa mpangilio wa mfuatano unaotarajiwa wa utekelezaji. Mengi tayari yanaendelea kutekelezwa kwa namna fulani.

1. Kukamilisha na kutekeleza MAP, ambayo itaongozwa na Idara ya Usafiri na Uhamaji
2. Kutekeleza mabadiliko yafuatayo ya ubadilishaji wa maeneo wa kabla ya marekebisho:
  - a. Kuhalalisha Vitengo vya Makazi ya Nyongeza (ADU) karibu na jiji zima
  - b. Kupunguza au kuondoa masharti ya chini zaidi ya maegesho ya barabarani kwa matumizi mengi
  - c. Kurekebisha masharti ya ulinzi wa miti
3. Kubuni Mpango wa Ujenzi wa Makazi ili kutambua aina za makazi zinazohitajika zaidi na zinazopaswa kupewa kipaumbele kulingana na mwelekeo na makadirio ya kidemografia.
4. Kutetea na kutenga rasilimali za uwezo wa utekelezaji wa idara ndani ya Ofisi ya Mtendaji wa Maendeleo ya Uchumi na Idara ya Huduma za Ukaguzi ili kuongoza juhudi zilizoainishwa kupitia mchakato huu.
5. Kufanya tathmini ya uwezo na mahitaji ya miundombinu
6. Kuanzisha urekebishaji wa kina wa ubadilishaji wa maeneo katika jiji lote

Mara baada ya hatua hizi sita kuu kukamilika, Mpango wa Sasa | wa Baadaye unapaswa kuangaliwa upya na mapendekezo yaliyosalia yapewe kipaumbele kwa utekelezaji. Wakati huo huo, idara nyingine na washirika wa jumuiya wanapaswa kutumia mfumo wa mpango, vichwa vya mpango, na mwongozo wa sera mahususi kama nyenzo ili kuhakikisha upatanishi wa Worcester ya Sasa | ya Baadaye kwa juhudi za utekelezaji sambamba

na zilizoratibiwa. Hizi ni baadhi ya njia ambazo wakaazi na washirika wanaweza kutumia kuchukua hatua katika kutekeleza mpango huu:

**Kusaidia ongezeko la uwezo wa idara** ndani ya Ofisi Kuu ya Maendeleo ya Kiuchumi na ndani ya Idara ya Huduma za Ukaguzi ili kutekeleza mabadiliko na kutekeleza utiifu.

**Kuendelea kushirikiana na kuongoza wengine** kwa kuwakumbusha kuwa mapendekezo ya Worcester ya Sasa | ya Baadaye yana msingi wake katika miaka miwili ya uchambuzi na mchakato na jumuiya. Kusaidia kuhakikisha kuwa mazungumzo ni yenye kulenga na yenye kujenga kadri Jiji linavyopiga hatua mbele hadi kiwango kinachofuata cha maelezo na kuanza kukabiliana na maelewano na mivutano kwa njia zinazoonekana zaidi na zinazoweza kuhusishwa.

**Chagua malengo na mapendekezo unayoweza kuchangia kutekeleza** ambayo umeunganishwa na kuwekeza nayo, wasiliana na idara husika ya Jiji, na utumie mpango huu kama mwongozo wa kusukuma kipengele hicho cha mpango mbele kwa kutumia mtazamo, ujuzi, uwezo na ushawishi ambao unapaswa kutoa.

Kwa utetezi, uongozi, mipango, na kazi ya wanajumuiya na taasisi husika na mashirika yanayoshirikiana maono ya Worcester ya Sasa | ya Baadaye, tunaweza kusukuma mbele utekelezaji kwa pamoja kutoka kila kona ya Worcester.